

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Dar es Salaam.
03 Desemba, 2025

Barua pepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekutana na kufanya mazungumzo na Naibu Mwenyekiti wa Biashara wa Jumuiya ya Madola na Baraza la Uwekezaji (CWEIC), Lord Hugo Swire, tarehe 02 Desemba, 2025, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo yao, wamejadiliana kuhusu kuanzisha ushirikiano wa kibiashara na fursa za uwekezaji zinazoweza kuchochea ukuaji wa uchumi na ajira nchini.

Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Serikali imefungua milango kwa wawekezaji wenye nia ya kushirikiana na Tanzania katika kusukuma mbele ajenda ya maendeleo ya Taifa, na kuongeza kuwa kwa zaidi ya miongo sita Tanzania imeendeleza ushirikiano thabiti na wawekezaji na wadau wa maendeleo, huku ikiimarisha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara.

Akigusia matukio ya uvunjifu wa amani ya tarehe 29 Oktoba, 2025, Rais Dkt. Samia amesitiza kuwa Tanzania inaendelea kuwa nchi yenye utulivu na ina mifumo madhubuti ya kushughulikia masuala yake ya ndani.

Aidha, ameihakikishia jumuiya ya wawekezaji kuwa Serikali itaendelea kuwajibika kwa usalama wa wawekezaji na biashara zao, na kudokeza kuwa nchi ipo katika hatua za awali za mchakato wa mapitio ya Katiba unaokusudiwa kuimarisha utendaji wa taasisi na sekta ya biashara na uwekezaji.

Kwa upande wake, Lord Swire ameonesha utayari wa CWEIC kuendeleza ushirikiano na Tanzania kama mshirika wa kimkakati ili kuvutia wawekezaji zaidi kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola.

Halikadhalika, amemshukuru Rais Dkt. Samia kwa mapokezi na kumtakia heri katika kuendeleza juhudi za kuimarisha uchumi wa nchi, huku akiiombea Tanzania kurejea katika hali ya utulivu.



[Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano /](#)
[ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania /](#)
[ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania](#)



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Taarifa Zaidi:

Lord Hugo Swire ni Naibu Mwenyekiti wa Biashara wa Jumuiya ya Madola na Baraza la Uwekezaji CWEIC na aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza. Swire, ambaye ni mwanachama wa House of Lords, ni mbobezi katika masuala ya diplomasia, biashara na masuala ya Jumuiya ya Madola.

Kuhusu CWEIC:

Commonwealth Enterprise and Investment Council (CWEIC) ni mtandao rasmi wa biashara wa Jumuiya ya Madola unaojumuishia nchi 56, na unalenga kuimarisha biashara na uwekezaji kupitia ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na taasisi za maendeleo, pamoja na kuhamasisha fursa za kiuchumi ndani ya nchi wanachama.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Kissu'.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

